# 斯瓦希里语高级阅读

北 京 广 播 学 院 非 通 用 语 系 列 教 材



# Maandishi Mbalimbali ya Kiswahili

陈元猛 编

北京广播学院出版社

北京广播学院非通用语系列教材

# 斯瓦希里语高级阅读



陈元猛 编

北京广播学院出版社

图书在版编目（CIP）数据

斯瓦希里语高级阅读/陈元猛编. —北京：北京广播学院出版社，2004.2

ISBN 7-81085-273-6/K·131

Ⅰ.斯… Ⅱ.陈… Ⅲ.斯瓦希里语—阅读教学—教材 Ⅳ.H823.94

中国版本图书馆CIP数据核字（2004）第012767号

**斯瓦希里语高级阅读**

编　　者：陈元猛

责任编辑：蔡开松

出版发行：北京广播学院出版社

社　　址：北京市朝阳区定福庄东街1号　邮编：100024

电　　话：010-65738557　65738538　传真：010-65779405

网　　址：http://www.cbbip.bbi.edu.cn

经　　销：新华书店总店北京发行所

印　　刷：北京金华印刷有限公司

开　　本：730×988毫米　1/16

印　　张：37.5

印　　次：2004年2月第1版　2004年2月第1次印刷

ISBN 7-81085-273-6/K·131　　定价：88.00元

版权所有　翻印必究　印装错误　负责调换

# 前　言

自 1960 年秋季起，北京广播学院外语系（即今北京广播学院国际传播学院）率先在我国高等学校开设斯瓦希里语专业，至今 40 多年过去了。

由于种种原因，在我国开办斯瓦希里语等非通用语专业是非常不易的，比如师资力量，有些从零开始，有些则十分薄弱；外文原著更加匮乏。到目前为止，我国也只有一套由外语教学与研究出版社于 1991 年出版的斯瓦希里语基础教材——《斯瓦希里语》（1～4 册），供低年级学生使用。因此，很有必要编出一本可供斯瓦希里语专业高年级学生，甚至硕士研究生使用的斯语高级阅读文本，以帮助其逐步提高阅读能力，增强斯语语感，养成斯语使用者的思维逻辑、审美情趣、欣赏习惯等。

编者在我国斯瓦希里语界广大同仁的帮助下，特别是得到中国外文出版发行事业局人民画报社领导的大力支持和斯瓦希里文部温炳文、郑于铭等同志的鼎力相助，在充分占有原版斯文图书的基础上，经过三年多的阅读、比较、遴选，终于编成《斯瓦希里语高级阅读》（Maandishi Mbalimbali ya Kiswahili）一书。本书分政经篇（包括论非洲社会主义，坦桑尼亚临时宪法，执政党——革命党诞生的过程，国家法律，对外政策，经济发展概况，国家发展历史沿革，以及地理风貌、环境保护、战争等论述）；文学篇（包括中短篇小说全文或节选、散文美文、书评、剧本选、现代诗歌选、人物传记等）。内容主要是从纯语言角度去选取，力争做到内容原汁原味，文体多种多样，风格各具特色，照顾国家及地域差别，使读者从中领略非洲人民的人文风貌，喜怒哀乐，纯朴心灵，及社会众生相等。其选录的文章，有些说理透彻，深入浅出，一语中的，给读者以深刻启迪与警醒；有些则形象生动，惟妙惟肖，匠心独运，读后令人拍案叫绝。

本书是在目前国内斯文图书资料十分匮乏，经费有限，且有钱也难订购得到的情况下，编者采取的一种应急措施与权宜之计。根据需要，编者

只对原文中少数用词不当的地方，以及一些拼写错误进行了部分订正。

斯瓦希里语是非洲三大语言之一，主要应用于东非、中非各国，包括坦桑尼亚、肯尼亚、乌干达，以及刚果（金）、布隆迪、卢旺达、赞比亚、莫桑比克、马拉维、科摩罗、索马里、埃塞俄比亚、苏丹等国及周边广大地区。据联合国教科文组织一份材料称，世界上已有近两亿人讲此种语言，并有很大的发展空间，是一种朝阳语言。

本书的出版，使我长长地舒了一口气，算是我自1961年起从事斯瓦希里语专业学习、工作和教学、科研40余年来所进行的一个小结，做出的一个交代，画上的一个句号，了却的一个心愿。这也是我之所以在没有经济回报的情况下却乐此不疲、默默劳作的原因。

由于编者水平比较有限，又力不从心，所搜集到的原文材料的种类比较单一，水平参差不齐，年代也较久远，本书一定存在不少缺点与不足，烦请读者在学习中自己去校正，去琢磨，去剖析，去品味。凡不懂之处，可向各位从事斯语工作的师长及有关外籍专家、驻华使馆工作人员、在华留学生、词典、同学、朋友等请教，相互切磋，共享读书的乐趣。只有多读，精思，联系上下文，加上一点别的技巧，恐怕有时会无师自通。编者在学习或教学工作中多数时候也是这样行事的。你说呢，亲爱的新老读者朋友们！

这里，我要衷心感谢北京广播学院高福安副院长从大局出发，对此书出版的关怀与支持，衷心感谢北京广播学院国际传播学院蔡帼芬院长、杨秀文副院长、徐琴媛副院长的支持与帮助，教务处黄凯副处长的热心督促，及教材科张贵科长的周到服务，北京广播学院出版社蔡翔社长、闵惠泉总编以及蔡开松主任等的关照与辛劳。

同时，我还要对在此书的排版过程中付出了辛勤劳动的北京天恒明远激光照排公司的同志们，对参加此书校对工作的北京广播学院国际传播学院2000级斯瓦希里语·英语专业班全体学生，对在书稿准备工作中资料室申克宾同志给予的热情帮助等，一并表示感谢。

在北京广播学院2004年即将迎来50周年校庆之际，谨以此书作为我敬献给为其服务了整整一辈子的北京广播学院的一份薄礼。

陈元猛

2003－12－01



此为试读，需要完整PDF请访问：www.ertongbook.com

# Yaliyomo ndani yake

**Ujamaa** ········ Julius K. Nyerere( 1 )
**Katiba ya Muda ya Tanzania 1965** ········ Jamhuri ya Muungano wa Tanzania( 8 )
**Azimio la Arusha** ········ Halmashauri Kuu ya TANU( 20 )
**Shabaha Ni Mwanadamu** ········ Julius K. Nyerere( 34 )
**Utekelezaji wa Azimio la Arusha** ········ Julius K. Nyerere( 42 )
**Kuzaliwa kwa CCM** ········ Ali A. Mohamed( 62 )

* * * * *

**Sheria za Mikataba** ········ Iyob N. Kawamala( 75 )
**Kesi za Ndoa na Talaka** ········ N. E. R. Mwakasungula(101)

* * * * *

**Harakati ya Kitabaka Katika Afrika** ········ Kwame Nkrumah(117)

* * * * *

**Ana kwa Ana na Rais Nyerere** ··· David Martin(Maswali), Julius K. Nyerere(Majibu)(126)
**Hotuba ya Rais Kuhusu Siasa ya Nchi za Nje Kwenye Mkutano Mkuu wa TANU, Mwanza**, 1967 ········ Idara ya Habari(132)
**Uchumi Bora** ········ Peter Temu(147)
**Uchumi(3)—Urithi Wetu** ········ S. Ndunguru(164)
**Rushwa** ········ F. Malangalila(169)

* * * * *

**Historia ya Tanzania Kabla ya 1880** ········ Wizara ya Elimu ya Tanzania(184)
**Tanzania Kabla na Baada ya Uhuru** ········ Chuo Kikuu cha Dar es Salaam(191)
**Mapambano ya Ukombozi Zanzibar** ········ B. F. Mrina, W. T. Mattoke(197)
**Jiografia ya Tanzania—Urithi Wetu** ········ S. Ndunguru(216)
**Hifadhi ya Wanyama na Ndege wa Afrika** ········ B. S. Swebe, H. W. D. Longden(229)
**Vita vya Kagera** ········ J. F. Ngatuni, A. N. Kigadye, M. A. I. Ghahae(250)

* * * * *

**Mikononi Mwa Mauti** ········ Nerbert Chiduo(264)
**Operesheni Vipusa** ········ Dadi M. Mwaware(304)
**Gamba la Nyoka** ········ E. Kezilahabi(320)
**Kaburi Bila Msalaha—Hadithi ya Vita vya Mau Mau** ········ P. M. Kareithi(362)
**Mpira wa Miguu au Mazingaombwe?** ········ J. E. Makaidi(373)

* * * * *

**Kielezo cha Insha** ······ Shaaban Robert(383)

* * * * *

**Maisha Yangu na Baada ya Miaka Hamsini** ······ S. D. Kiango, T. S. Y. Sengo(423)
**Wahusika wa Shaaban Robert** ······ A. N. Shija(438)
**Maisha ya Shaaban Robert na Mawazo Yake** ······ M. A. Maganga(442)

* * * * *

**Mashairi ya Mwamko wa Siasa** ······ L. N. Honero, T. Y. Sengo, S. Y. Ngole(459)

* * * * *

**Machozi ya Mwanamke** ······ I. S. Ngozi(465)
**Kifo Kisimani** ······ Kithaka wa Mberia(479)

* * * * *

**Mashujaa wa Afrika** ······ M. B. Sanga(497)
**Patrice Lumumba** ······ H. A. K. Mwenegoha(Mfasiri)(509)
**Kwame Nkrumah** ······ M. W. Kanyama Chiume(Mfasiri)(528)
**Idi Amin** ······ H. A. K. Mweneoha, J. P. Mbonde(552)
**Edward Moringe Sokoine** ······ B. S. Swebe(572)

# Ujamaa

*Julius K. Nyerere*

Ujamaa, kama demokrasi, ni moyo. Katika nchi ya Ujamaa kama unataka kuhakikisha kwamba watu wanajali shida za watu wengine, linalotakiwa ni mawazo ya Kijamaa, wala siyo kufuatisha tu utaratibu maalum wa siasa. Shababa ya kitabu hiki ni kufikiria tabia hiyo; wala siyo kueleza utaratibu unaotakiwa kuendesha Ujamaa katika mataifa ya kisasa.

Mtu binafsi, au hata taifa, utalitambua kama ni taifa la Ujamaa au si la Ujamaa kwa tabia yake. Ujamaa hauhusiani hata kidogo na mtu kuwa na mali au kutokuwa na mali. Maskini wanaweza kuwa na roho za kibepari—wanyonyaji wa binadamu wenzao. Vile vile, tajiri anaweza akawa na roho ya Ujamaa; anaweza akathamini mali yake kwa sababu tu inaweza kutumiwa kuwasaidia binadamu wenzake. Lakini mtu anayetumia mali kwa shabaha ya kuwatawala wenzake wo wote ni bepari. Na vivyo hivyo atabesabiwa mtu anayetamani kutumia mali namna hiyo, kama akipata nafasi !

Nimesema kuwa tajiri anaweza akawa mpenda Ujamaa. Lakini kumpata tajiri mpenda Ujamaa ni shida sana. Kwa kweli utajiri na Ujamaa hupingana. Lakini kuwako kwa matajiri maana yake si lazima kwamba nchi yao ni tajiri. Matajiri wanaweza kupatikana katika nchi maskini sana kama Tanganyika, kama vile vile wanavyoweza kupatikana katika nchi tajiri kama Marekani. Maana utajiri wa namna hiyo hautokani na uhodari wa mtu, wala utajiri wa nchi, ila hutokana na ugawaji usio wa haki wa mali inayopatikana. Kwa hiyo, ingawa tajiri anaweza akawa mpenda Ujamaa, lakini ni shida kwa nchi ya Ujamaa kuzaa matajiri.

Kwa kuwa kupatikana kwa matajiri hakutokani na nchi zao kuwa tajiri, wataalamu wa tabia za binadamu watashangaa watakapojaribu kutafuta kwa nini nchi zetu za Kiafrika hazikuwa na matajiri ? Maana tulikuwa tunayo mali ya kutosha kupata matajiri wa Kiafrika. Nadhani watagundua kwamba, kwa sababu ya utaratibu wa jadi za nchi za Kiafrika, ugawaji wa mali inayopatikana haukutoa nafasi ya unyonyaji. Huenda vile vile wakasema kwamba, kwa sababu ya tabia hiyo, Afrika haikuweza kutoa makabaila wakaao bure, na kwa hiyo hakukupatikana mtu wa kujifunza mambo ya sanaa au sayansi ambayo nchi za kikabaila zinajivunia. Lakini sanaa au mafanikio ya sayansi ni mazao ya ubongo wa binadamu ambayo, kama ardhi, ni moja ya baraka za Mungu kwa binadamu. Na mimi siwezi kuamini kwamba Mwenyezi Mungu ni mjinga kiasi hicho, cha kufanya moja ya baraka zake zitegemee unyonyaji na uharibifu wa mtu mwingine. Watetezi wa ubepari wanadai

kwamba mali ya tajiri ni ujira wa haki kwa ajili ya uwezo wake au mawazo yake. Lakini dai hili halithibitishwi na mambo yalivyo. Mali ya tajiri haitegemei sana fikara au uwezo wa tajiri mwenyewe, kama vile vile ambavyo mamlaka ya sultani hayategemei juhudi, mawazo au akili yake. Wote ni watumizi na wanyonyaji wa uwezo na mawazo ya watu wengine. Hata ukipata tajiri mwenye akili na mwenye bidii sana, tofauti baina ya mawazo yake, juhudi yake, na kazi yake, na juhudi ya watu wengine, haiwezi kufanana hata kidogo na tofauti zilizopo baina ya mapato yao. Ikiwa katika nchi moja kuna mtu mmoja, hata akiwa mjanja na mwenye juhudi namna gani, na mtu huyo mapato yake ni sawa na mapato ya wenzake elfu nzima, basi nchi hiyo, bila shaka, ina walakini.

Kujilimbikizia mali kwa sababu ya kujipatia mamlaka au hadhi si mawazo ya Ujamaa. Katika nchi ya namna hiyo mali inawaharibu mioyo wale wanaoipata. Mali inawapa hamu ya kuishi kwa raha zaidi kuliko wenzao, kuvaa mavazi bora zaidi, na kuwazidi kwa kila njia. Wanaanza kutamani kupanda ngazi juu zaidi iwezekanavyo kuwashinda wenzao. Ili waifaidi mali yao, lazima tofauti baina ya starehe zao na shida za wenzao nchini zionekane; na hivyo basi huanza mashindano ya kutaka kutajirika—na jambo hilo ni kinyume cha Ujamaa.

Mtu kujilimbikizia mali matokeo yake huwa ya kibepari. Lakini si hivyo tu, hata mtu kutamani kulimbikiza mali katika nchi ya Ujamaa, mtu huyo atatiliwa shaka. Maana kama kijiji kimetengenezewa utaratibu ambao shida za kila mtu zinafikiriwa, basi mradi kila mtu anafanya kazi, hakuna hata mtu mmoja katika kijiji kile atakayekuwa na wasiwasi hata akajilimbikizia mali kwa kujiandaa na shida za kesho. Kijiji chenyewe kingepaswa kumtunza, au kumtunza mkewe kama yeye akifariki, au watoto wake. Hivi ndivyo vijiji vilivyokuwa vikifuata jadi ya Kiafrika vilivyofanikiwa kufanya. Katika kijiji cha Kiafrika, watu wote, tajiri na maskini, walikuwa salama kabisa. Mikasa ilileta njaa, lakini njaa hiyo ilikuwa ikimpata kila mtu, tajiri na maskini. Hakuna aliyekuwa na shida, ama ya njaa, ama ya hadhi, kwa sababu tu yeye binafsi hakuwa na mali; aliweza kutegemea kabisa mali waliyokuwa nayo wenziwe katika kijiji ambamo yeye naye anaishi. Huo ulikuwa Ujamaa. Huo ndio Ujamaa. Hakuwezi kuwapo Ujamaa wa kujilimbikizia mali, maana kufanya hivyo kutabitilafiana na tafsiri ya neno lenyewe. Ujamaa unashikilia zaidi kugawana au kushirikiana mapato. Haja ya Ujamaa ni kuhakikisha kwamba wale wanaopanda wanavuna mavuno ya haki ya yale wanayopanda.

Kuunda mali, kama kwa kutumia maarifa ya kisasa, ama maarifa ya kizamani, kunahitaji vitu vitatu. Kwanza, ardhi. Mwenyezi Mungu ametupa ardhi, na kutoka katika ardhi tunapata vitu tunavyovitengeneza kupata mahitaji yetu. Pili, vifaa. Pole pole tumegundua kwamba vifaa vina faida. Kwa hiyo tunatengeneza jembe, shoka, au trekta, au kiwanda, kutusaidia kuunda mali; yaani vitu tunavyovihitaji. Na tatu, tunahitaji juhudi ya mwanadamu, yaanikazi. Hatuna haja ya kusoma vitabu vya Karl Marx au Adam Smith kugundua kwamba jembe au ardhi peke yake haiwezi kuleta mali. Wala hatuna haja ya kupata shahada ya Uchumi kufahamu kwamba ardhi haiundwi na mfanya kazi wala kabaila. Ardhi ni

zawadi ya Mwenyezi Mungu kwa mwanadamu, ipo siku zote. Bila ya kupata shahada ya Uchumi, tunafahamu vile vile kwamba shoka na plau yametengenezwa na mfanya kazi. Yaelekea kwamba baadhi ya rafiki zetu walioendelea hawana budi kusoma sana ili tu hatimaye wagundue kwamba babu zetu walitengeneza mashoka ya mawe ili kuwarahisishia kazi ya kuwachuna paa waliowaua kwa marungu, ambayo pia walijitengenezea wenyewe!

Katika vijiji vya asili vya Kiafrika, kila mmoja ni mfanya kazi. Hakukuwako njia nyingine ya kuishi katika kijiji kile. Hata mzee wa kijiji, ambaye anaonekana anastarehe tu bila ya kufanya kazi yo yote , ambaye anaonekana kwamba anafanyiwa kazi na kila mtu kijijini, kwa kweli enzi za ujana wake alifanya kazi sana. Mali aliyo nayo hivi sasa haihesabiwi kuwa yake binafsi; ni yake tu kwa sababu yeye ni mzee wa kijiji, na wananchi wa kijiji kile ndio walioichuma mali ile. Yeye ni mdhamini tu. Mali hiyo haikumpa hadhi wala mamlaka. Vijana humheshimu tu kwa sababu yeye ni mzee kuliko wao, na amekitumikia kijiji kile kwa muda mrefu zaidi. Wazee maskini waliheshimika namna ile ile kama wazee tajiri.

Ninaposema kwamba katika vijiji vya asili vya Kiafrika kila mtu ni mfanya kazi, sina maana ya kusema kwamba hakukuwako matajiri wanaoajiri wengine tu, ila vile vile hawakuwako malofa wala wazururaji ovyo. Moja katika mafanikio makubwa ya ujamaa wetu wa asili ni kwamba kila mtu alikuwa analindwa, na kila mtu alikuwa anakarimiwa sana. Lakini mara kwa mara tunasahau siku hizi kwamba msingi wa mafanikio hayo ni huu: ilikuwa inaaminika kwamba kila mtu alikuwa akifanya kazi inayompasa ya kuchuma mali, isipokuwa labda watoto, wagonjwa na vikongwe tu. Bepari au kabaila hakujulikana katika vijiji vyetu vya Afrika vya zamani. Si hivyo tu, wala hatukuwa na wanyonyaji wa aina ya sasa: malofa, wazururaji, ambao wanatarajia ukarimu wa wenzao kama haki yao, lakini wenyewe hawafanyi kazi yo yote kulipa ukarimu ule! Unyonyaji wa kibepari haukuwezekana. Lakini vile vile ulofa na uzururaji ilikuwa aibu kubwa.

Baadhi yetu tunaosema habari za maisha ya Kiafrika, na ambao tunajivunia, kwa haki kabisa, kuendelezwa kwa ukarimu wetu ambao ni sehemu ya maisha ya Kiafrika, itatufaa tukumbuke ile methali ya Kiswahili isemayo, *Mgeni siku mbili; ya tatu mpe jembe.* Kwa kweli inawezekana mgeni mwenyewe akaomba jembe hata kabla mwenyeji hajampa, maana alijua alichotarajiwa kufanya, na angeona aibu kuendelea kukaa bure. Kwa hiyo kufanya kazi, ambako kulikuwa sehemu ya maisha, ndiko kulikokuwa msingi wa mafanikio hayo ya ujamaa ambayo sasa tunajivunia.

Hakuna Ujamaa bila ya kazi. Nchi inayoshindwa kuwapa wananchi kazi inawazuia wasipate ujira wa haki wa mazao ya juhudi na jasho lao, nchi hiyo ina haja ya kurekebishwa. Vile vile, mtu ambaye anaweza kufanya kazi, na amepewa na umma njia za kufanya kazi, na halafu asifanye kazi, mtu huyo ana hitilafu. Hana haki kutarajia kupata cho chote kutoka kwa umma, kwa sababu yeye mwenyewe hatii kitu.

Maana nyingine ya mfanya kazi, akiwa mtu *mwenye* kuajiriwa, yaani kinyume cha tajiri, inaonyesha mawazo ya kibepari, yaliyoletwa Afrika wakati ulipokuja ukoloni na ni

neno geni katika mawazo yetu ya Kiafrika. Hapo kale Mwafrika kamwe hakutamani awe na mali kwa shababa ya kuwakandamiza wenzake. Hakuwa na vibarua au manamba wa kumfanyia kazi. Lakini baadaye wakaja mabepari wa kigeni. Walikuwa matajiri. Walikuwa na nguvu. Na hivyo Mwafrika naye akatamani kuwa tajiri. Hakuna la ajabu mtu kutamani kuwa tajiri; wala si vibaya mtu kutamani kupata nguvu inayoletwa na mali. Lakini hakika ni vibaya sana, ikiwa tunatamani kupata mali na nguvu hizo ili tuitumie kuwakandamiza watu wengine. Kwa bahati mbaya, baadhi yetu tumekwisha kujifunza kutumia mali kwa sababu hiyo, na ambao tungependa kutumia njia anazotumia bepari kupata mali na nguvu hiyo. Yaani, baadhi yetu tunatamani kuwatumia au kuwanyonya ndugu zetu kwa sababu ya kujijenga sisi wenyewe. Hili ni wazo geni kwetu, na linapingana na mawazo ya Ujamaa tunayotaka kuyajenga hapa kwetu.

Kwa hiyo hatua yetu ya kwanza lazima iwe kubadili mawazo yetu, turudie tena mawazo yetu ya zamani. Katika vijiji vyetu vya zamani vya Kiafrika tuliishi katika jumuia. Sisi tuliwaangalia wananchi wa kijiji, na wao wakatuangalia sisi. Hatukutamani kuwanyonya wananchi wenzetu; wala haja hiyo haikuwako.

Na wakati tunapoyakataa mawazo ya kibepari yaliyoletwa katika Afrika na ukoloni, lazima vile vile tukatae na utaratibu wa kibepari ulioleta mawazo hayo. Moja katika utaratibu huo ni mtu kumiliki ardhi, ikawa yake. Kwetu sisi Waafrika ardhi siku zote ilijulikana kuwa mali ya umma. Kila mtu katika kijiji alikuwa na haki ya kutumia ardhi, maana bila ya hivyo hakuwa na njia ya kupata riziki yake; na haiwezekani mtu awe na haki ya kuishi bila ya kuwa na haki ya kupata njia za kutafutia riziki. Lakini haki ya Mwafrika katika ardhi ni haki *ya kuitumia tu*; hakuwa na haki zaidi ya hiyo, wala haikuingia akilini kudai haki zaidi ya hiyo.

Wakoloni wakaleta mawazo tofauti kabisa; wakafanya ardhi kuwa ni kitu cha kuuzwa. Katika utaratibu huo, mtu angeweza kudai sehemu ya ardhi kuwa mali yake binafsi; *aitumie au asiitumie si kitu*. Mimi ningeweza kujichukulia pande la ardhi, nikaliita 'langu'; halafu nikajiondokea kwenda kwenye mwezi. Kazi ambayo ningetakiwa kuifanya, ili nijipatie riziki kutoka katika ardhi 'yangu', ni kuwatoza kodi watu ambao wanataka kuitumia. Kama ardhi hii iko mjini, sina haja hata ya kujenga. Ningewaachia wapumbavu wanaotaka kujenga katika sehemu zilizo karibu na kiwanja changu, na hivyo bei ya kiwanja changu itapanda. Halafu nikarudi kutoka katika mwezi, nikawakamua wajinga hawa wanilipe ada kubwa sana kwa sababu ya ardhi yangu, na thamani hiyo wameipandisha wenyewe wakati ambapo mimi nilikuwa nikistarehe mwezini! Utaratibu huo ni mgeni kwetu: tena ni wa ovyo. Makabaila katika nchi inayoamini kuwa ardhi inaweza kuwa mali ya mtu binafsi wanaweza wakawa (na kwa kweli ndivyo walivyo kwa kawaida) sawa na wale wazururaji niliokuwa nikiwasema: wanyonyaji wakubwa.

Tusikubali wazuke wanyonyaji hapa kwetu Tanganyika. Serikali ya TANU lazima irudie utaratibu wa jadi ya Kiafrika wa kumiliki ardhi. Ndiyo kusema kwamba mtu atakuwa na haki ya kushika ardhi *wakati anapoitumia*. Utaratibu wa mtu kumiliki, ikawa yake



此为试读,需要完整PDF请访问: www.ertongbook.com

tu na ya warithi wake wakati wote hata kama hawaitumii, lazima ukomeshwe. Utaratibu huo unafanya ardhi iuzwe kama nguo, na unaleta unyonyaji. Kama nilivyokwisha sema, hatuna budi kurudia tena fikara zetu za zamani, Ujamaa wetu wa jadi ya Kiafrika na kuutumia katika vijiji vipya tunavyovijenga sasa. TANU imeamua kuufanya Ujamaa kuwa msingi wa siasa yake katika kila jambo. Watu wa Tanganyika wametupa ruhusa ya kuitekeleza siasa hiyo, kwa kuichagua Serikali ya TANU iwaongoze. Kwa hiyo Serikali inaweza kutazamiwa kutunga sheria yoyote inayolingana na misingi ya Ujamaa.

Lakini, kama nilivyokwisha sema hapa mwanzo, Ujamaa wa kweli ni mawazo ya mtu. Kwa hiyo ni juu ya watu wa Tanganyika, wakulima, wafanya kazi, wanafunzi, viongozi, wote sisi, kuhakikisha kwamba mawazo hayo ya Kiujamaa hayapotoshwi kwa sababu ya vishawishi vya shibe ambayo mtu binafsi anaweza akaipata, au kwa kushawishia kuona faida ya umma kuwa si kitu kwa kulinganisha na shibe ya kikundi cha watu wachache.

Kama ambavyo katika vijiji vyetu vya zamani, mzee aliheshimika kwa sababu ya umri wake na kazi yake aliyoitenda katika kijiji, vile vile katika vijiji vya sasa tutailinda heshima hiyo ya umri na utumishi mrefu katika nchi. Zamani mali ya mzee aliyeonekana kuwa tajiri kwa kweli ilikuwa mali ya umma aliyokabidhiwa kuidhamini. Vile vile hata leo mali ambayo inaonekana kuwa viongozi wanayo kwa sababu ya vyeo walivyopewa, inaweza kuhesabiwa kuwa yao tu kwa sababu inawafaa katika kutimiza kazi zao. Ni "chombo" walichokabidhiwa na umma kwa faida ya watu wanaowatumikia. Si yao binafsi; na hawawezi kutumia sehemu yo yote ya mali hiyo kama njia ya kujilimbikizia mali zaidi kwa faida yao binafsi, wala kujikinga na shida katika siku ambazo hatakuwa na cheo hicho tena. Kufanya hivyo itakuwa kuharibu imani ya wale wanaowadhaminia. Kama wazee hawa wameutumikia umma wakati wa ujana wao, basi ni juu ya umma kuwaangalia wakati ambapo hawawezi tena kufanya kazi.

Katika vijiji vyetu vya zamani, mtu au ukoo katika kabila alikuwa tajiri au maskini kama kabila zima ni tajiri au maskini. Kama kabila lilikuwa na maendeleo, basi kila mtu katika kabila lile alipata faida ya maendeleo hayo. Leo Tanganyika ni nchi maskini. Hali ya maisha ya umma iko chini kiasi cha kuaibisha. Lakini kama kila mtu katika nchi, mke kwa mume, atatambua hayo na kufanya kazi ukomo wa nguvu zake, kwa faida ya nchi nzima, basi Tanganyika itaendelea; na maendeleo hayo kila mtu atayapata.

Lakini mafanikio hayo lazima *yagawanywe* kwa watu wote. Mtu mwenye kuamini Ujamaa kikwelikweli hawezi kuwanyonya wenzake. Kwa hiyo, ikiwa kikundi cha watu katika nchi yetu watasema kuwa kwa kuwa wanaleta faida kubwa zaidi katika uchumi wa nchi, basi wajichukulie sehemu kubwa zaidi ya mazao hayo kuliko hata wanavyohitaji; na kama waking 'ang' ania kufanya hivyo ingawa kwa kufanya hivyo watapunguza sehemu yao katika uchumi wa nchi, na hivyo watapunguza hatua ya maendeleo yatakayoufaidia umma, basi kikundi hicho kinanyonya, au kinajaribu kunyonya, binadamu wenzao. Kinaonyesha mawazo ya kibepari.

Lazima yatakuwako makundi fulani ambayo kwa sababu ya thamani ya mazao wanayo-

lima au vitu wanavyotengeneza, watatia mali nyingi zaidi katika uchumi wa nchi kuliko wengine. Lakini wale wengine pia wanaweza wakawa wanatengeneza vitu au wanalima mazao *kiasi* kile kile, au pengine zaidi, lakini kwa bahati mbaya haina *bei* kubwa kwa wakati huo. Kwa mfano: chakula anachokilima mkulima kina manufaa zaidi kwa watu kuliko almasi inayochimbwa Mwadui. Lakini mchimba almasi wa Mwadui anaweza akadai, kwa haki kabisa, kwamba kazi yake inaingiza fedha zaidi katika *nchi* kuliko *mkulima*. Lakini kama wakiendelea kudai kwamba wapate faida yote wao peke yao, na hata sehemu isitumike kumsaidia mkulima, basi hao wana mawazo ya kibepari!

Hapo ndipo tabia ya mtu inapohesabiwa katika Ujamaa. Shabaha moja ya kuwa na Vyama vya Wafanya Kazi ni kuhakikisha kwamba wafanya kazi wanapata malipo ya haki ya kazi zao. Lakini ujira wa haki lazima uwe wa haki kwa nchi nzima. Kama ujira huo ni mkubwa kuliko kiasi ambacho nchi inakimudu bila ya kuwapatisha taabu wananchi wengine, basi ujira huo si wa haki. Viongozi wa Vyama vya Wafanya Kazi, na wanachama wao, kama wanaamini Ujamaa kweli, hawatakuwa na haja ya kulazimishwa na Serikali kuweka madai yao ya mishahara katika kima ambacho haja za umma zitakiweka. Lakini kama kuna wenye mawazo ya kibepari miongoni mwao, basi Serikali ya Ujamaa italazimika kuingilia kati na kuwazuia wasiyatumie mawazo yao ya kibepari.

Kama ilivyo katika vikundi, ndivyo ilivyo kwa watu binafsi. Kuna utaalamu au ujuzi fulani ambao kwa sababu fulani unawafanya wale walio nao wapate mshahara mkubwa zaidi kuliko watu wengine. Lakini hata hapo mtu mwenye kuamini Ujamaa kweli kweli atadai ujira kwa kazi yake ambao anajua kuwa ni wa haki kwa kulinganisha na utajiri au umaskini wa nchi yake ambamo yeye anaishi. Hataweza kulazimisha nchi yake kumlipa mshahara sawa na ule unaopatikana katika nchi tajiri zaidi, isipokuwa kama mawazo yake ni ya kibepari.

Ujamaa wa Ulaya ulitokana na mapinduzi ya kilimo, na mapinduzi ya viwanda yaliyokuja baada ya hapo. Mapinduzi ya kilimo yalileta tabaka za makabaila na wasio na ardhi; na yale ya viwanda yalileta bepari na mfanya kazi wa viwandani.

Mapinduzi hayo yalipanda mbegu za uhasama katika nchi, na uhasama huo ndio uliozaa Ujamaa wa Ulaya. Si hivyo tu, ndio pia uliofanya mashahidi wa Ujamaa wa Ulaya wautengeneze Ujamaa katika mawazo yanayokubalika. Vita havikuonekana tena kuwa kitu kibaya, au mkasa, lakini vilihesabiwa kuwa na faida, na vya lazima. Kama sala ilivyo kwa Mwislamu au Mkristo, vivyo hivyo ndivyo ilivyokuwa ikihesabiwa vita kwa wale waaminio Ujamaa wa Ulaya: shababa ya kuleta usawa. Kila kimoja katika hivyo kinakuwa na msingi wa maisha yote ya Ujamaa. Mtu mwenye kuamini Ujamaa wa Ulaya hawezi kuufikiria Ujamaa wake bila ya kufikiria baba wa Ujamaa huo, yaani Ubepari!

Lazima niseme kuwa mimi niliyelelewa katika Ujamaa wa Kiafrika naona kuwa upinzani huu ni wa ovyo kabisa. Unaujenga ubepari na kuupa hadhi ambayo ubepari wenyewe hauidai wala hauistahili. Maana maneno yenyewe karibu ni sawa na kusema, 'Bila Ubepari, na uhasama unaoleta katika nchi, hakuwezi kuwako Ujamaa!' Narudia *tena*

kusema kwamba watu wanaoamini Ujamaa wa Ulaya kuutukuza ubepari namna hii ni jambo la ovyo.

Lakini kwa upande mwingine, Ujamaa wa Kiafrika haukupata faida ya Mapinduzi ya Kilimo au Mapinduzi ya Viwanda. Haukuanzishwa na kuwapo na uhasama wa tabaka za watu katika nchi. Na kwa kweli, wala sidhani kuna neno linalofanana na 'tabaka' katika lugha zetu za makabila, maana lugha hueleza tabia za wale wanaoisema, na tabia ya 'tabaka' haiko katika makabila ya Kiafrika.

Shababa na msingi wa Ujamaa wa Kiafrika ni ukoo. Mtu mwenye kuamini Ujamaa wa Kiafrika kweli kweli hawaoni watu wa tabaka fulani kama ndugu zake na tabaka nyingine kuwa adui zake. Haungani na wale anaowaita ndugu zake ili awateketeze wale ambao si ndugu zake. Afadhali awahesabu watu wote kuwa ndugu zake: kama watu wa ukoo wake. Ndiyo sababu kifungu cha kwanza cha Imani ya TANU kinasema, 'Binadamu wote ni ndugu zangu, na Afrika ni moja'.

Kwa hiyo 'Ujamaa' unaeleza mawazo yetu. Unapinga ubepari, ambao shabaha yake ni kuunda nchi zenye raba kwa msingi wa kunyonyana. Vile vile unapinga aina ya Ujamaa unaotarajia kujenga nchi zenye raha, katika msingi wa uhasama baina ya mtu na mtu.

Sisi tulio katika Afrika hatuna haja ya kufundishwa Ujamaa, kama vile vile ambavyo hatuna haja ya kufundishwa demokrasi. Yote hayo tunayo katika jadi zetu, katika makabila yetu yaliyotulea. Ujamaa wa Kiafrika wa leo unaweza kujifunza kutoka jadi zetu za kutambua umuhimu wa umma, kama vile vile ambavyo zamani tulitambua umuhimu wa ukoo. Lakini sasa haiwezekani kuufikiria Ujamaa katika mipaka ya ukoo, au ya kabila, au hata ya taifa peke yake. Maana Mwafrika anayeamini Ujamaa hawezi akachora mstari katika ramani akasema, 'Watu walio upande huu ni ndugu zangu, lakini wale walio upande ule hawana haki na mimi'. Kila mtu katika ulimwengu huu ni ndugu yake.

Wakati tulipokuwa tunapigania kumwondoa mkoloni, tulijifunza faida za Umoja. Tulitambua kwamba mawazo yale yale ya Kiujamaa ambayo katika siku za zamani za makabila yalimpa kila mtu usalama kwa sababu ya kuwa sehemu ya ukoo fulani, lazima yahifadhiwe na kutumiwa katika ukoo mkubwa zaidi wa taifa zima. Lakini tusiishie hapo. Kutambua kwetu kwa faida ya umoja katika ukoo lazima kuelekezwe mbali zaidi: zaidi ya kabila, zaidi ya taifa, au zaidi ya bara zima: mpaka wamejumlishwa binadamu wote. Hilo ndilo lengo lililo dhabiri la Ujamaa wa kweli.

# Katiba ya Muda ya Tanzania 1965

*Jamhuri ya Muungano wa Tanzania*

## Sura ya I

Jamhuri ya Muungano, Chama na Watu

### Sehemu ya I

Jamhuri ya Muungano na Chama

1. Tanzania ni Utawala wa Jamhuri ya Muungano.

2. —(1) Nchi zilizomo ndani ya Tanzania ni Tanganyika na Zanzibar, pamoja na bahari za nchi hizo.

(2) Mamlaka ya kutengeneza Sheria yaweza kuruhusu Tanzania igawanywe katika mikoa, wilaya na maeneo mengineyo.

3. —(1) Kutakuwako Chama kimoja cha siasa katika Tanzania.

(2) Mpaka vitakapoungana Chama cha TANU na Chama cha Afro-Shirazi (ambayo vitakapokuwa vimeungana vitaunda hicho Chama kimoja cha Siasa), Chama cha Tanganyika kitakuwa TANU, na Zanzibar kutakuwa na Chama cha Afro-Shirazi.

(3) Shughuli zote za kisiasa katika Tanzania, zisizokuwa zile ambazo zinahusika na vikao vya Serikali ya Jamhuri ya Muungano, vikao vya Utawala na Baraza la kutunga Sheria la Zanzibar, au Serikali za mitaa kama zitakazowekwa na sheria au chini ya sheria iliyowekwa na mamlaka ya kutengeneza sheria, shughuli hizo zitafanywa kwa kusimamiwa au chini ya usimamizi wa Chama hicho.

(4) Ile katiba iliyoko katika Nyongeza ya Kwanza ya Katiba hii itakuwa ndio Katiba ya TANU, na Katiba hiyo itaweza kubadiliwa mara kwa mara (na ndani yake kufanywa sharti kuhusu muungano wa TANU na Chama cha Afro-Shirazi na yatakayofuata) kwa mujibu wa masharti yaliyomo katika Katiba hiyo kuhusu muungano huo.

### Sehemu ya II

Watu

4. —(1) Kila raia wa Tanzania aliyefikia umri wa miaka ishirini na moja, ila kama kwa Sheria ya Bunge Kuu ameondoshewa sifa ya kuweza kuandikishwa kupiga kura, raia huyo, atakapofika mahali palipochaguliwa na mnamo wakati uliowekwa kwa ajili ya kuan-

dikisha kupiga kura, atakuwa na haki ya kuandikishwa kuwa mpiga kura, kwa ajili ya uchaguzi unaofanywa na Watu, na hakuna mtu wa namna nyingine mwenye haki ya kuandikishwa hivyo.

(2) Kila mtu anayeandikishwa kama ilivyokwishaelezwa ila kama Sheria ya Bunge Kuu imemuondoshea sifa ya kupiga kura, mtu huyo atakapofika mahali palipochaguliwa na mnamo wakati uliowekwa kwa ajili ya kupiga kura, atakuwa na haki ya kupiga kura kwenye uchaguzi unaofanywa na Watu katika sehemu ya Tanzania ambayo ameandikishwa apige kura, na hakuna mtu wa namna nyingine mwenye haki ya kupiga kura hiyo:

Isipokuwa kwamba Sheria ya Bunge Kuu yaweza kumruhusu mtu aliyeandikishwa kupiga kura katika sehemu moja ya Tanzania apige kura katika sehemu nyingine ya Tanzania kwenye uchaguzi wa mjumbe wa Bunge wa jimbo ikiwa yeye ni mgombea uchaguzi wa sehemu hiyo na pia ataruhusiwa kupiga kura katika sehemu hiyo nyingine kwenye uchaguzi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano unaofanywa wakati ule ule wa uchaguzi wa mjumbe wa jimbo, na hakuna kitu katika kifungu hiki kitakachofahamika kwamba kinamzuia mtu ye yote asipige kura katika sehemu nyingine yo yote badala ya kupiga kura katika sehemu aliyoandikishwa apige kura.

(3) Hakuna Sheria ya Bunge Kuu itakayoruhusu raia ye yote wa Tanzania aondoshewe sifa ya kuweza kuandikishwa kuwa mpiga kura katika uchaguzi unaofanywa na Watu, au itakayoruhusu kuondoshewa sifa ya kupiga kura kwa mpiga kura ye yote aliyeandikishwa kwenye uchaguzi huo, isipokuwa kwa sababu za kuwa yeye ni raia wa Nchi nyingine hana akili timamu, ana makosa, mabaya, hayuko katika nchi, kashindwa kuthibitisha umri wake, uraia au kuandikishwa kwake.

(4) Kwa kufuata masharti ya Katiba hii, uandikishaji wa wapiga kura kwa uchaguzi unaofanywa na Watu na upigaji kura kwenye uchaguzi huo utarekebishwa na Sheria ya Bunge Kuu na uandikishaji huo na uchaguzi huo, kwa mujibu wa Katiba hii na Sheria yo yote ya Bunge Kuu kuhusu uandikishaji na upigaji kura, utaendeshwa chini ya maagizo na usimamizi wa Tume ya Uchaguzi.

5. Kila raia wa Tanzania aliyefikia umri wa miaka kumi na nane na ambaye anaikubali imani, shabaha na madhumuni ya Chama kama yalivyoelezwa katika Katiba ya Chama, baada ya kulipa ada na michango iliyoruhusiwa katika Katiba ya Chama, atakuwa na haki ya kuwa mwanachama wa Chama.

## Sura ya II

Rais wa Jamhuri ya Muungano

6.—(1) Kutakuwako Rais wa Jamhuri ya Muungano atakayekuwa ni Mkuu wa Serikali na vile vile Jemadari Mkuu wa Majeshi ya Vita.

(2) Katika utendaji wa shughuli zake, Rais atatenda kwa kadri anavyotaka yeye mwenyewe wala hatakuwa na wajibu wa kufuata shauri atakalopewa na mtu ye yote, ila atakaporuhusiwa na sheria iwe kinyume cha hivyo.

7. —(1) Rais atachaguliwa na Watu kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii na kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Bunge Kuu juu ya urekebishaji wa uchaguzi wa Rais, kwa kufuata katiba hii.

(2) Uchaguzi wa Rais utafanywa wakati wo wote ambao moja wapo ya matukio yanayofuata litakapotokea, ndio kusema—

(a) Bunge Kuu litakapovunjwa;

(b) Rais atakapokufa;

(c) Rais atakapojiuzulu bila ya kulivunja Bunge Kuu kwanza;

(d) Iwapo, kwa kufuata fungu la 9 la Katiba hii, Jaji Mkuu atathibitisha kwamba Rais hawezi kufanya shughuli zake na, ikawa ndani ya muda wa miezi sita itakayofuatia hakuuondoa uthibitisho huo.

(3) Ndani ya muda wa siku hamsini wa kuvunjwa kwa Bunge Kuu, au siku ishirini na moja tangu kutokea tukio lo lote jingine litakaloleta sababu ya kufanywa uchaguzi wa Rais, Mkutano wa Uchaguzi wa Chama, utakaofanywa kwa mujibu wa masharti ya Katiba ya Chama kuhusu uchaguzi huo, utakutana; na Mkutano wa Uchaguzi huo utamteuwa raia mmoja wa Tanzania aliyefikia umri wa miaka thelathini na ambaye ni mwanachama wa Chama awe ni mgombea peke yake wa uchaguzi wa Rais.

(4) Mgombea uchaguzi wa Rais huyo aliyeteuliwa na Mkutano wa Uchaguzi atatajwa ili achaguliwe na watu ambao watapiga kura ya kumkubali au kumkataa mgombea uchaguzi huyo; na ikiwa, katika kumpigia kura huko—

(a) kura nyingi zimemkubali mgombea uchaguzi huyo, basi mtu huyo atachaguliwa kuwa Rais na Tume ya Uchaguzi itatamka kuchaguliwa kwake;

(b) kura nyingi hazikumkubali mgombea uchaguzi huyo, basi mtu huyo hatachaguliwa kuwa Rais; na Mkutano wa Uchaguzi utamteuwa mtu mwingine awe ni mgombea peke yake wa uchaguzi wa Rais kwa mujibu wa kifungu cha (3), na uchaguzi utafanywa kwa mujibu wa kifungu hiki kuhusu mgombea uchaguzi huyo.

(5) Iwapo mtu ametamkwa na Tume ya Uchaguzi kuwa amechaguliwa awe Rais, basi kuchaguliwa kwake hakutaulizwa katika mahakama yo yote.

8. —(1) Rais ataanza kushika kazi siku itakayofuatia baada ya kutamkwa kuwa amechaguliwa; na, ila kama atakufa au atajiuzulu mapema sana, ataendelea kudumu katika kazi yake mpaka mtu atakayechaguliwa kuwa Rais kwenye uchaguzi utakaofuata wa Rais atakapoanza kushika kazi hiyo.

(2) Wakati atakapoanza kazi yake, Rais ataapa kiapo cha uaminifu, na kiapo kingine chochote kinachohusika na utendaji wa kazi yake; kama inavyoweza kuainiwa ndani ya Sheria ya Bunge.

9. —(1) Kila itakapokuwa kiti cha Rais kiwazi, au Rais hayupo katika Tanzania, au Jaji Mkuu amethibitisha, kwa kutumia hiari yake baada ya kupokea uamuzi wa Baraza la Mawaziri kumuomba atumie uwezo wake kuhusu jambo hilo na baada ya kufikiria ushahidi



此为试读,需要完整PDF请访问: www.ertongbook.com